# 8. Viua wadudu ghushi na visivyo halali

## Mada ya 8d

## Wajibu wa serikali na wauza pembejeo za kilimo

# JARIDA LA UHAKIKA

## 8. Viua wadudu ghushi na visivyo halali

## <u>Mada ya 8d:</u> Wajibu wa serikali na wauza pembejeo za kilimo

**Pembejeo ghushi na zisizo halali za kilimo** sio tu shida barani Afrika bali duniani kote. Bidhaa hizi huagizwa nchini kutoka nchi za nje au zinatengenezwa ndani ya nchi. Shida hii haiwaathiri tu wakulima na watumiaji bali pia inaathiri wauza pembejeo na serikali. CropLife International, IFDC na mashirika mengine ya pembejeo za kilimo yameungana katika vita dhidi ya pembejeo ghushi na zisizo halali. Lakini serikali na wauza pembejeo za kilimo pia wanaweza kuchangia katika wajibu faulani katika vita hivi.

**Serikali inaweza kufanya nini ili kukomesha pembejeo ghushi na zisizo halali katika eneo hili?**

- **Utungaji Sheria**: Sheria na taratibu huleta nguvu za kisheria za kukomesha bidhaa ghushi na zisizo halali kuingia nchini. Inatakiwa iwepo orodha ya bidhaa zinazokubalika nchini na viambato vinavyofaa kuwa katika bidhaa hizo
- **Utekelezaji wa sheria**: Sheria na taratibu zatakiwa kutekelezwa na kutumika ndio ziwe na nguvu. Vitengo na wakala wengi hujishughulisha na kutekeleza sheria.
- **Usimamizi wa mipaka**: Bidhaa ghushi na zisizo halali huingia nchini kwa kupitia mipakani kwa barabara au baharini. Kwa kukagua mipaka yote bidhaa ghushi na zisizo halali zitazuiwa kuingia nchini.
- **Usajili na thibitisho kwa wauza bidhaa za kilimo**: Usajili wa wauzaji utaepusha wauzaji walaghali na haramu. Kama wauzaji wanajulikana, ni rahisi kudhibiti wanavyouza.
- **Uelimishaji na ufahamisho**: Wakulima, wauza pembejeo za kilimo, maafisa wa serikali na wateja lazima wafahamu kuwepo kwa madhara ya bidhaa ghushi na zisizo halali ili wachukue hatua inayofaa.

**Wauzaji wa bidhaa za kilimo wanaweza kufanya nini ili kukomesha pembejeo ghushi na zisizo halali katika eneo hili?**

- **Kanuni za maadili mema**: Wauzaji wa pembejeo za kilimo wanatakiwa kufuata kanuni za maadili mema za kimataifa iliotengenezwa na shirika la chakula na kilimo la umoja wa kimataifa (FAO). Kanuni hizo za maadili mema zinasema kuwa muuzaji bidhaa atajishughulisha tu na bidhaa halisi na halali. Mashirika ya wauza pembejeo za kilimo yanahitaji wanachama kuweka sahihi ya kufuata kanuni za maadili mema.

- **Ushiriki wa habari**: Mikutano ya mara kwa mara kati ya serikali na washika dau wengine yafaa iandaliwe ili kupata habari, kushiriki tajriba na kujifunza kutoka kwa makosa yao.
- **Mfumo wa kulinda wanaokosoa**: Ulindaji wa wanaoripoti biashara haramu na wakosaji inahakikisha wanaojihusisha na bidhaa ghushi na zisizo halali wameripotiwa na kuadhibiwa.
- **Mafunzo**: Wakulima, wauza pembejeo za kilimo na maafisa wa serikali wanatakiwa kufunzwa kuhusu bidhaa ghushi na zisizo halali na jinsi ya kuzitambua.

# MWONGOZO

## 8. Viua wadudu ghushi na visivyo halali

## Mada ya 8d: Wajibu wa serikali na wauza pembejeo za kilimo

### Vifaa vinavyohitajika:

- ☑ Ubao ulio na makaratasi
- ☑ Markers (1 nyeusi, 1 bluu, 1 kijani, 1 nyekundu)
- ☑ Kadi za rangi

### Muda unaohitajika: Dakiki 30

### Maandalizi:

- ☑ Karatasi ilio na kichwa: *Wajibu wa serikali na wauza pembejeo za kilimo*
- ☑ Kadi za rangi zilizo na vichwa:
  - *Serikali*
  - *Wauza pembejeo za kilimo*

# Mwanzo

**U**sikivu: Waambie washiriki kwamba sasa tumejifunza maana ya pembejeo ghushi na zisizo halali, kwa nini zipo sokoni, na madhara ya kuziuza na kuzinunua. Uliza ni nani anayeamini kwamba yeye kama muuzaji pembejeo za kilimo anaweza kuajibika kwa kupigana dhidi ya bidhaa ghushi na zisizo halali. Wacha wainue mikono yao.

**K**ichwa: Waambie washiriki kichwa huku ukiwaonyesha karatasi iliyo na kichwa**:** *Wajibu wa serikali na wauza pembejeo za kilimo*

**K**usadikika: Elezea uzoefu wako katika pembejeo ghushi na zisizo halali za kilimo.

**M**alengo: Kufafanua wajibu wa serikali na wauza pembejeo za kilimo katika vita dhidi ya pembejeo ghushi na zisizo halali.

**M**anufaa: Ukifahamu ni nini unaweza kufanya kama muuza pembejeo za kilimo, unaweza kusaidia katika kupigana na hii shida ya pembejeo ghushi na zisizo halali.

**M**welekeo: Katika kipindi hiki, hatutafafanua wajibu wa kila mshika dau katika vita dhidi ya pembejeo ghushi na zisizo halali; tutaangazia tu wajibu wa serikali na wauza pembejeo za kilimo.

# Wasilisho

## **U**fafanuzi, **M**aonyesho, **M**azoezi, na **M**wongozo:

1. Waambie washiriki kwamba kuna **washika dau** tofauti katka vita dhidi ya pembejeo ghushi na zisizo halali za kilimo kama CropLife International, tasnia ya mbolea, IFDC, mashirika ya wauza pembejeo za kilimo, serikali na wakulima.
2. Waambie washiriki kwamba tutachemsha bongo kuhusu maswali yafuatayo: **Serikali** yaweza kufanya nini ili kukomesha biashara ya pembejeo ghushi na zisizo halali za kilimo? Jaribu kuuliza maswali kama serikali itafanya nini kudhibiti uingizaji wa pembejeo ghushi na zisizo halali za kilimo nchini? Je, sheria zilizoko zinatosha kukomesha biashara ya pembejeo ghushi na zisizo halali? Serikali inawezaje kudhibiti wanaouza pembejeo za kilimo? Kudhibiti huku kutasaidiaje katika kupigana na biashara hii.
3. Andika majibu yote kwa karatasi. Hakikisha kwamba hoja zifuatazo zimetajwa:
   - **Utungaji Sheria**: Sheria na taratibu huleta nguvu za kisheria za kukomesha bidhaa ghushi na zisizo halali kuingia nchini. Inatakiwa iwepo orodha ya bidhaa zinazokubalika nchini na viambato vinavyofaa kuwa katika bidhaa hizo
   - **Utekelezaji wa sheria**: Sheria na taratibu zatakiwa kutekelezwa na kutumika ndio ziwe na nguvu. Vitengo na wakala wengi hujishughulisha na kutekeleza sheria.
   - **Usimamizi wa mipaka**: Bidhaa ghushi na zisizo halali huingia nchini kwa kupitia mipakani kwa barabara au baharini. Kwa kukagua mipaka yote bidhaa ghushi na zisizo halali zitazuiwa kuingia nchini.
   - **Usajili na thibitisho kwa wauza bidhaa za kilimo**: Usajili wa wauzaji utaepusha wauzaji walaghali na haramu. Kama wauzaji wanajulikana, ni rahisi kudhibiti wanavyouza.
   - **Uelimishaji na ufahamisho**: Wakulima, wauza pembejeo za kilimo, maafisa wa serikali na wateja lazima wafahamu kuwepo kwa madhara ya bidhaa ghushi na zisizo halali ili wachukue hatua inayofaa.

   **Kumbukumbu:** Hoja zilizotajwa hapo juu ni mwongozo tu na washiriki wanaweza kutaja hoja muhimu sana kutoka eneo lao.

4. Endelea na swali lifuatalo: Ni nini wauza pembejeo za kilimo wanaweza kufanya ili kukomesha biashara ya pembejeo ghushi na zisizo halali za kilimo? Uliza maswali

ya kusisimua washiriki ili watoe mawazo kama: Polisi watajuaje kuna biashara haramu inaendelea? Serikali itajuaje kuna shida tatizo la bidhaa ghushi au zisizo halali? Itasaidia kama wakulima na maafisa wa mipaka watajua jinsi ya kutambua bidhaa ghushi na zisizo halali?

5. Andika majibu yote kwenye karatasi na uhakikishe hoja zifuatazo zimetajwa:
   - **Kanuni za maadili mema**: Wauzaji wa pembejeo za kilimo wanatakiwa kufuata kanuni za maadili mema za kimataifa iliotengenezwa na shirika la chakula na kilimo la umoja wa kimataifa (FAO). Kanuni hizo za maadili mema zinasema kuwa muuzaji bidhaa atajishughulisha tu na bidhaa halisi na halali. Mashirika ya wauza pembejeo za kilimo yanahitaji wanachama kuweka sahihi ya kufuata kanuni za maadili mema.
   - **Ushiriki wa habari**: Mikutano ya mara kwa mara kati ya serikali na washika dau wengine yafaa iandaliwe ili kupata habari, kushiriki tajriba na kujifunza kutoka kwa makosa yao.
   - **Mfumo wa kulinda wanaokosoa**: Ulindaji wa wanaoripoti biashara haramu na wakosaji inahakikisha wanaojihusisha na bidhaa ghushi na zisizo halali wameripotiwa na kuadhibiwa.
   - **Mafunzo**: Wakulima, wauza pembejeo za kilimo na maafisa wa serikali wanatakiwa kufunzwa kuhusu bidhaa ghushi na zisizo halali na jinsi ya kuzitambua.

<u>**Kumbukumbu:**</u> Hoja zilizotajwa hapo juu ni mwongozo tu na washiriki wanaweza kutaja hoja muhimu sana kutoka eneo lao.

# Malizia

**M**uhtasari: Toa muhtasari kwa kurudia kile serikali na wauza pembejeo za kilimo wanaweza kufanya ili kukomesha biashara ya pembejeo ghushi na zisizo halali.

**M**aswali: Uliza kama kuna yeyote aliye na swali au maoni.

**T**athmini: Waulize serikali yaweza kufanya nini ili kukomesha biashara katika pembejeo ghushi na zisizo halali. Wauzaji pembejeo za kilimo wanaweza kufanya nini ili kukomesha biashara katika pembejeo ghushi na zisizo halali?

**H**atua fuatilizi: Kwa vile sasa unajua la kufanya, chukua hatua bora. Njia mwafaka ya kufanya hivi ni kupitia mashirika ya wauza pembejeo za kilimo. Wapatie changamoto ya kuchukua hatua.

Sambaza **makaratasi ya taarifa ya maelezo** kwa washiriki wote.

CropLife
AFRICA MIDDLE EAST

IFDC